

## MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



### TAARIFA KWA UMMA

18 FEBRUARI, 2018

#### UKAGUZI MAALUM WA DAWA NA VIFAA TIBA ULIOFANYWA NA TFDA KANDA YA KATI

1. Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura Na. 219 yenye jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa Chakula, Dawa, Vipodozi, Vifaa tiba na Vitendanishi.
2. TFDA inapenda kuutaarifu umma kuwa kati ya tarehe 5 hadi 7 Februari, 2018 ilifanya ukaguzi maalum wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika Halmashauri za Manispaa za Dodoma, Morogoro, Singida na Halmashauri za Wilaya za Manyoni, Iramba, Gairo, Mvomero, Kongwa na Chamwino.
3. Ukaguzi huo ulilenga kubaini uwepo wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi bandia, duni, ambavyo havijasajiliwa na vya serikali vilivyosambazwa kanda ya kati.
4. Jumla ya maeneo **172** yalikaguliwa ambapo **48** ni famasi za dawa za binadamu, **5** ni famasi za dawa za mifugo, **3** ni hospitali, **3** ni vituo vya afya, **76** ni maduka ya dawa muhimu za binadamu, **30** ni maduka ya dawa muhimu za mifugo, **1** ni zahanati na **6** ni vituo vya huduma za tiba za mifugo (Veterinary centres).
5. Katika ukaguzi huo jumla ya makopo 12 ya dawa bandia aina ya Ascillin (Ampicillin 250mg Capsules) ya kopo la ujazo wa kapsuli 1,000 yenye taarifa zinazoonesha imetengenezwa na kiwanda cha Astra Lifecare (India) Pvt. Ltd ilibainika. Dawa hiyo bandia inatofautiana na dawa halisi iliyosajiliwa na Mamlaka. Tofauti hizo ni :-

Na.	Halisi	Bandia
1.	Muda wa matumizi wa dawa hii uliothibitishwa na mtengenezaji ni miaka miwili. Toleo halisi ni namba 390 ambalo limetengenezwa tarehe <b>05/2015</b> na muda wake wa kuisha	Muda wa matumizi wa dawa hii uliooneshwa kwenye lebo ni miaka mitatu. Toleo bandia ni namba 390 limetengenezwa <b>04/2016</b> na muda wake wa kuisha

	matumizi ni tarehe <b>04/2017.</b>	matumizi ni tarehe <b>03/2019.</b>
2.	Maandishi ya kuonesha tarehe ya kutengeneza, tarehe ya mwisho wa matumizi na namba ya toleo yameandikwa kwa 'Dot matrix printer'.	Maandishi ya kuonesha tarehe ya kutengeneza, tarehe ya mwisho wa matumizi na namba ya toleo yameandikwa kwa maandishi ya kawaida(not doted)
3.	Maandishi ya jina la kibiashara la dawa limeandikwa kwa herufi zilizo wima (ascillin)	Maandishi ya jina la kibiashara la dawa limeandikwa kwa herufi zilizoegemea upande wa kulia
4.	'Artwork cord' kwenye lebo ya dawa halisi ni UT-CL-108A- <b>6</b>	'Artwork cord' kwenye lebo ya dawa bandia ni UT-CL-108A- <b>8</b>
5.	Kona za lebo ya dawa halisi ziko 'curved'	Kona za lebo za dawa bandia zina 'edge'

6. Aidha, matokeo ya uchunguzi wa kimaabara yanaonesha kuwa dawa ya Ascillin ya kapsuli kutokidhi vigezo vya muonekano wa dawa (physical appearance) tofauti na ile iliyosajiliwa hususan kwenye kifungashio cha dawa.
7. Baadhi ya dawa zenye ubora duni zilizobainika katika ukaguzi huo ni pamoja na Ampimax suspension ya Reyoung Pharmaceuticals Ltd, China toleo Na. 151272 iliyokuwa imeganda, Penizen V suspension toleo Na. DD7001 ya kiwanda cha Zenufa Laboratories Ltd, Dar Es Salaam iliyokuwa imeganda na Co-malather tablets toleo Na. 170005 ya Shelys Pharmaceuticals Ltd.
8. Thamani ya dawa na vifaa tiba hivyo vilivyokamatwa ni shilingi **2,927,000/=** kama ifuatavyo;

Na.	Dawa	Aina	Thamani (TZS)
1.	Dawa bandia	1	540,000/=
2.	Dawa zenye ubora duni	4	128,000/=
3.	Dawa za Serikali ya Tanzania zilizokutwa katika maduka ya watu binafsi	2	38,000/=
4.	Dawa ambazo hazijasajiliwa	9	2,221,000/=

9. Maeneo yafuatayo yalikutwa na dawa za Serikali ya Tanzania kinyume na sheria;

- a) Duka la Bi. Ernea Mwandembele, Mvumi – Chamwino, Dodoma
- b) Kelly Pharmacy, Manispaa ya Morogoro

10. Vilevile, wakaguzi waliweza kubaini makosa mbalimbali kama vile maduka kutoa huduma za tiba za hospitali kinyume na sheria, maduka kutokuwa na vibali, dawa zilizoisha muda wa matumizi kukutwa kwenye rafu (shelves), maduka ya dawa muhimu kukutwa na dawa zisizoruhusiwa katika maduka hayo.
11. Baada ya ukaguzi katika maeneo husika hatua mbalimbali zilichukuliwa na TFDA kama ifuatavyo:-
- i) Maduka yaliyokutwa na dawa za Serikali, bandia na kutokuwa na vibali yalifungwa na utaratibu wa kisheria umeshaanza ambao unashirikisha Jeshi la Polisi na Baraza la Famasi.
  - ii) Kuchukua dawa bandia, duni, zisizosajiliwa na zile za Serikali kwa hatua zaidi za uchunguzi na hatimaye kuchukua hatua za kisheria. Majarida ya upelelezi yenye namba SI/RB/1212/2018 na SI/RB/949/2018 yamefunguliwa mkoani Singida.
  - iii) Maeneo mengine yaliyokutwa na makosa zaidi ya yaliyoainishwa hapo juu yalitakiwa kutoa maelezo na hatua za marekebisho walizofanya kabla ya hatua stahiki hazijachukuliwa na TFDA kwa kushirikiana na mabaraza ya kitaaluma.
  - iv) Kutoa maelekezo ya kurasimisha biashara kwa wale ambao hawakuwa na vibali.
  - v) Kutoa elimu ya umuhimu wa kuzingatia sheria.
12. Kutokana na kubainika kwa matoleo ya dawa bandia na duni yaliyotajwa hapo juu, Mamlaka inautahadharisha umma, wafanyabiashara pamoja na watoa huduma za afya kama ifuatavyo:-
- a) Hospitali, vituo vya afya na zahanati zote za serikali ambako dawa hii bandia imeonekana zinaelekezwa kutoendelea kutoa dawa hii kwa wagonjwa na kurudisha makopo Bohari ya Dawa kwa ajili ya uteketezaji.
  - b) Wale wote ambao wamepewa dawa husika zilizotajwa wanaelekezwa kuzirudisha walikopewa
  - c) Kutoa taarifa Mamlaka ya Chakula na Dawa wanapohisi kuuziwa dawa duni, bandia au zilizoisha muda wa matumizi.
13. Aidha, TFDA na Jeshi la Polisi linapiga marufuku matangazo ya vipodozi yanayotolewa kwenye mitandao ya kijamii kwa kuwa yanapotosha Umma. TFDA hutoa vibali vya matangazo kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii iwapo waombaji wataomba.
14. Nimwombe sasa ASP Joshua Mwangasa Mkuu wa kitengo cha Cybercrime aweze kutoa maelezo kuhusiana na matangazo ya vipodozi kwenye mitandao ya kijamii.

15. Pamoja na maelezo ya ASP Mwangasa naomba niendeele kuisisitiza kwamba Mamlaka inaendelea kufuatilia ubora, usalama na ufanisi wa dawa na vifaa tiba vyote vilivyopo kwenye soko kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219 pamoja na kanuni zake na endapo zitaonekana kutokidhi vigezo vya ubora na usalama hatua za kisheria zitachukuliwa.
16. Wito unatolewa kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa pale wanapo baini uwepo wa dawa duni na bandia kwenye soko pamoja na wale wanaouza kwa kificho vipodozi bila vibali hasa maeneo ya majumbani ambayo hayajaidhinishwa na TFDA.

**Imetolewa na;  
Kaimu Mkurugenzi Mkuu,  
Mamlaka ya Chakula na Dawa,  
S.L.P 77150,  
Dar es Salaam.**

**Simu: +255 22 2452108/2450512/2450751/658 445222/777 700 002/685 701735**

**Nukushi: +255 22 2450793**

**Baruapepe: [info@tfda.go.tz](mailto:info@tfda.go.tz)**

**Tovuti: [www.tfda.go.tz](http://www.tfda.go.tz)**